

# TAZAMA ninavyokua

Ifuatayo ni orodha ya ukaguzi ya kuona iwapo mtoto wako anafikia hatua za ukuaji hadi miaka mitatu ya maisha. Ufanisi wa uingiliaji kati unategemea kutambua mahitaji na kutoa huduma na msaada MAPEMA.

## MIEZI 0-4

- Anapeleka mikono kinywani
- Anajisukuma kwa mikono anapokuwa amelalia tumbo
- Anapokuwa amelala chali, anafikia vitu vya kuchezea vilivyoshikiliwa juu ya kifua chake
- Anajibingirisha kutoka chali kwenda kwa tumbo na kutoka kwa tumbo kwenda chali
- Anatoa sauti laini na anatabasamu
- Anatazama kwenye macho
- Anaweza kutulizwa kwa uzoefu kama vile kutikiswa

## MIEZI 5-8

- Anacheza na miguu yake
- Anaketi (anaweza kutumia mikono kujitegemeza anapokuwa amekaa)
- Anatumia sauti za konsonanti katika kubwabwaja
- Anaonyesha hamu ya chakula
- Anafurahia kushirikiana na wengine (kucheza mchezo wa kujificha)
- Anatumia mikono yote miwili kucheza na vitu vya kuchezea
- Anafuatilia vitu kwa macho

## MIEZI 9-12

- Anachukua vitu vidogo kwa kidole gumba na vidole
- Anatambua jina lake
- Anatumia ishara rahisi kama vile kutikisa kichwa kusema "hapana"
- Anajivuta kusimama kwa kushika samani
- Anasema “mama” na “dada” kwa njia yenye maana
- Anajilisha kwa vidole

## MIEZI 13-18

- Anatembea peke yake
- Anasaidia katika kuvishwa nguo
- Ana ratiba ya kawaida ya usingizi
- Anaiga maneno na vitendo rahisi
- Anashika na kunywa kutoka kikombeni
- Anaondoka karibu nawe, lakini anahakikisha upo karibu

## MIEZI 19-24

- Anakimbia
- Anapanda juu ya samani
- Anapiga mpira teke
- Anachora alama kwenye karatasi kwa penseli rangi
- Anatumia maneno 50 kufikia miezi 24
- Anatambua sehemu 5 za mwili
- Anatazama uso wako ili kuona jinsi ya kuitikia hali mpya

## MIEZI 24-36

- Anatumia maneno 2-3 kwa pamoja
- Anaelewa maagizo rahisi
- Anaweza kushiriki katika vikundi vidogo na watoto wengine
- Anaweza kutupa mpira na anajaribu kuushika anaporushiwa
- Anatumia uma



kadiri unavyojua **mapema**, ndivyo atakavyokua **vizuri zaidi**

# sisi NI NANI

Programu ya Watoto Wachanga na Wadogo ya North Carolina (ITP) inatoa huduma za ukuaji wa watoto wachanga na wadogo wenye mahitaji maalum, na familia zao. Mashirika Kumi na Sita ya Huduma za Ukuaji wa Watoto (CDSA) yanasimamia huduma hizi katika ngazi ya mtaa ili kuimarisha uwezo wa mtoto wako wa kukua na kuendelea.

Mtoto na familia wanaweza kupata msaada na huduma ikiwa mtoto:

- ana umri wa hadi miaka 3, na
- anachelewe kukua au ana hali iliyothibitishwa.



Kuchelewa kunaweza kuwa katika eneo moja au zaidi kati ya yafuatayo:

- kufikiri na kujifunza
- kutembea au kusogea, kuona, kusikia na afya
- kuelewa na kutumia sauti, ishara na maneno
- kuitikia na kujenga mahusiano
- kujitunza mwenyewe wakati wa kufanya mambo kama vile kula au kuvaa nguo

Mtoto mwenye hali iliyothibitishwa ana utambuzi wa jambo linaloweza kusababisha kuchelewa kukua. Hii inaweza kujumuisha matatizo ya kijenetiki, matatizo ya kuona, kupoteza uwezo wa kusikia au tawahudi.

Watoto wanaondoka kwenye ITP wanapotimiza miaka 3 au wanapokuwa hawahitaji tena huduma. Wanaenda shuleni, kwenye elimu maalum au programu nyingine za jamii. Kadiri unavyojua mapema mahitaji ya ukuaji wa mtoto wako, ndivyo atakavyokua vizuri zaidi kufikia uwezo wake kamili.

# tunafanya NINI

ITP inajumuisha msaada wa ufundishaji uliobuniwa kusaidia familia kukidhi mahitaji ya ukuaji ya mtoto wao mchanga au mdogo. Msaada na huduma za ITP zinatolewa katika mazingira ya jamii yanayotumiwa na watoto wote na ndani ya shughuli za kila siku za mtoto na familia.

## MAONO NA DHAMIRA YETU

Maono yetu kwa familia na walezi wa watoto waliosajiliwa katika Programu ya Watoto Wachanga na Wadogo ya NC ni kwamba wataweza kusaidia watoto wao kufikia uwezo wao wa juu kabisa.

Dhamira yetu ni kutoa msaada na huduma kwa familia na watoto ili kuwasaidia kufanikiwa nyumbani na katika jamii zao, kwa kutumia fursa za kujifunza za kila siku. Tutaheshimu utofauti wa familia na kutumia mbinu zinazotegemea ushahidi kuongoza kazi yetu.

# tunatoa HUDUMA GANI

Hizi hapa ni baadhi ya huduma zinazopatikana kusaidia mtoto wako na familia yako, ikihitajika:

- Tathmini
- Uratibu wa huduma
- Mafundisho maalum/Huduma za Ukarabati Zinazotegemea Jamii (CBRS)
- Tiba za kimwili, tiba za kazini na tiba za usemi-lugha
- Teknolojia saidizi
- Msaada wa familia
- Uuguzi na lishe

Tathmini, upimaji, na uratibu wa huduma za ITP hutolewa bila malipo kwako. Gharama za huduma nyingine za ITP zinatokana na kiwango cha ada kinachotegemea mapato. Medicaid na bima ya kibinafsi hutozwa kwa idhini yako. Mratibu wako wa Huduma atahakikisha unajua gharama yoyote inayohusika kabla ya huduma kuongezwa.



# nianze WAPI

Ikiwa una wasiwasi kuhusu ukuaji wa mtoto wako, usisubiri na kuangalia tu.

**WASILIANA NASI.** Piga simu, andika au tembelea CDSA yako ili kupeleka rufaa ya mtoto wako kwa ITP.

**PATA TATHMINI.** CDSA itafanya tathmini ya ukuaji ili kuona kama mtoto wako anastahili kupata huduma za ITP.

**SHIRIKI.** Familia yako itapewa mratibu wa huduma. Ikiwa mtoto wako anastahili kupata huduma za ITP, utasaidia kuandaa mpango wa huduma/msaada unaohitajika ili kumsaidia mtoto wako kufanikiwa.

**FANYA MAPEMA!** Kadiri unavyojua mapema, ndivyo atakavyokua vizuri zaidi!



# fanya HARAKA KUPELEKA RUFAA YA MTOTO WAKO




1. Mratibu wa huduma anaongoza familia yako katika mchakato wa rufaa.
2. Unatuambia kuhusu afya ya mtoto wako, anachokipenda, asichokipenda, uwezo wake na changamoto zake.
3. Tunafanya tathmini ya ukuaji ili kuamua kama mtoto wako anastahili kupata huduma za ITP.
4. Iwapo inakufaa, mratibu wa huduma atashirikiana nawe kuandaa Mpango Maalum wa Huduma za Familia (IFSP).
5. Huduma zilizoorodheshwa kwenye IFSP yako zitaanza ndani ya siku 30.
6. IFSP inabadilika kadri mahitaji ya mtoto wako na familia yako yanavyobadilika. IFSP inakaguliwa angalau kila miezi sita.
7. Mratibu wako wa huduma atakusaidia kupanga hatua za mbele mtoto wako anapoondoka katika ITP.

## afuta CDSA YAKO

CDSA hizi kumi na sita zinasimamia huduma za Programu ya Watoto Wachanga na Wadogo kwa watoto na familia katika kaunti zote 100 za NC.

1. **CDSA of Western NC • 828-250-3400**
   *Buncombe, Cherokee, Clay, Graham, Haywood, Henderson, Jackson, Macon, Madison, Swain and Transylvania*
2. **CDSA of the Blue Ridge • 828-278-6470**
   *Alleghany, Ashe, Avery, Mitchell, Watauga, Wilkes and Yancey*
3. **CDSA of the Cape Fear • Wilmington Office: 910-945-6021 • Fayetteville Office: 910-912-2200**
   *Bladen, Brunswick, Columbus, Cumberland, Duplin, New Hanover, Pender, Robeson and Sampson*
4. **CDSA of the Sandhills • 910-621-6200**
   *Anson, Harnett, Hoke, Lee, Montgomery, Moore, Richmond and Scotland*
5. **Concord CDSA • 704-998-5730**
   *Cabarrus, Iredell, Rowan, Stanly and Union*
6. **Durham CDSA • 984-250-1580**
   *Chatham, Durham, Franklin, Granville, Orange, Person, Vance and Warren*
7. **Greensboro CDSA • 743-902-5400**
   *Alamance, Caswell, Guilford, Randolph and Rockingham*
8. **Greenville CDSA • 252-737-1177**
   *Beaufort, Bertie, Greene, Hyde, Martin, Pitt and Wayne*
9. **Mecklenburg County CDSA • 704-336-7100**
10. **Morganton-Hickory CDSA • 828-433-5171**
    *Alexander, Burke, Caldwell, Catawba and McDowell*
11. **New Bern CDSA • 252-497-4175**
    *Carteret, Craven, Jones, Lenoir, Onslow and Pamlico*
12. **Elizabeth City CDSA • 252-338-4044** *Camden, Chowan, Currituck, Dare, Gates, Hertford, Pasquotank, Perquimans, Tyrrell and Washington*
13. **Raleigh CDSA • 919-664-1800 •** *Wake*
14. **Rocky Mount CDSA • 252-316-4800**
    *Edgecombe, Halifax, Johnston, Nash, Northampton and Wilson*
15. **Shelby CDSA • 980-552-4600**
    *Cleveland, Gaston, Lincoln, Polk and Rutherford*
16. **Winston-Salem CDSA • 336-713-7412**
    *Davidson, Davie, Forsyth, Stokes, Surry and Yadkin*

## *Maelezo Zaidi:*

**ncdhhs.gov/itp-beearly**



NC DEPARTMENT OF
HEALTH AND HUMAN SERVICES
Division of Child and Family Well-Being
NC Infant-Toddler Program (NC ITP)

www.ncdhhs.gov/itp-beearly

NCDHHS is an equal opportunity employer and provider. • 2/2024